



THE COUNTY ASSEMBLY OF LAMU

THE HANSARD

Wednesday, 15th April, 2026

*The Assembly met at the
Main Chambers, at 10:30 a.m.*

[Temporary Speaker (Hon. Beatrice Wamaitha Munge) in the Chair]

PRAYERS

Temporary Speaker (Hon. Beatrice Wamaitha Munge): Next Order.

Clerk-at-the-Table: Communication from the Chair

COMMUNICATION

Honourable members, may I take this opportunity to convey a message from H.E. the Governor to the Assembly regarding nomination for the appointment of a New Board Member for Lamu Public Service Board namely ADALLA AHMED ABUBAKAR via a letter dated 13TH March 2026 Ref No. CGL/C.S/1/12/VOL.II/24 received on 26TH March 2026. The above has been nominated by H.E. the Governor Pursuant to Section 58 of the County Government Act (2012).

Honourable members, having been forwarded to the County Assembly, the Assembly is therefore obligated to conduct approval hearings and make a determination of the nominee's suitability or otherwise as provided under the provisions of the Public Appointments (County Assemblies Approval) Act No. 5

of 2017. Therefore, I refer the name of the nominee and his curriculum vitae to the Committee on Appointment for vetting.

Honourable members, therefore, at this point I direct the Appointment Committee to consider extensive public participation as provided for in Article 118 of the Constitution as well as the Public Appointments (County Assemblies Approval) Act, 2017. I further advise the Committee to conclude its' report and submit the same to the Assembly to enable timely consideration and finalization within the stipulated timelines.

Honourable members, I therefore direct and wish the Appointment committee wisdom and resource to to the law and taking into account the larger interest of the County and its people. effectively and expediently reach conclusion on the matter guided by total fidelity

Thank you

Temporary Speaker (Hon. Beatrice Wamaitha Munge): Next Order.

Clerk-at-the-Table: Papers.

Hon. Bwana Mohamed Bwana(Majority Laeder): thank you honourable Speaker. Honourable Speaker, allow me to lay the following paper on the floor of the House;

1.Report of the Select Committee on the selection of members to serve in the Select Committees.

Temporary Speaker (Hon. Beatrice Wamaitha Munge): Next Order.

Clerk-at-the-Table: Motion.

MOTION

COUNTY OFFICIALS ENGAGING IN POLITICS WHILE IN OFFICE

Hon. Fahad Dini Adnan(Minority Leader): Thank you honourable Speaker.

Honourable Speaker, I beg to move the following motion:

THAT AWARE that County Government officers, including CECMs. Chief Officers, Ward Administrators, and support staff such as drivers, are employed to serve the people with neutrality, professionalism, and integrity.

FURTHER AWARE that the increasing involvement of these officers in partisan political activities while still holding

DEEPLY CONCERNED that such conduct undermines public confidence, distorts fair political competition, and leads to misuse of government resources for personal political gain.

NOTING THAT the Constitution of Kenya, under Article 10, enshrines national values of good governance, integrity, transparency, and accountability.

FURTHER NOTING that Article 232 provides for high standards of professional ethics. impartiality, and political neutrality in public service.

COGNIZANT of the provisions of the County Governments Act, which require county public officers to maintain discipline, professionalism, and avoid conduct that compromises service delivery;

ALSO GUIDED by the Public Officer Ethics Act, which clearly prohibits public officers from engaging in activities that conflict with their official duties or bring their office into disrepute.

This honourable house resolves;

1. THAT all County officials including CECMs, Chief Officers, Ward Administrators, and all staff must refrain from engaging in active politics while in office
2. THAT any officer wishing to participate in politics must resign, retire, or step aside in accordance with the law before engaging in any political activity.
3. THAT the County Public Service Board and relevant authorities enforce strict disciplinary action against any officer found using their position, government resources, or influence for political purposes.
4. THAT clear county guidelines be established to reinforce the separation between public service and political ambition.
5. THAT this House affirms that public office is not a campaign platform but a service to all citizens regardless of political affiliation.

Secunder

Hon. Bwana Mohamed Bwana(Majority Leader): Asante sana, Madam Speaker.

Madam Speaker, nimesimama kuunga mkono mswada uliowasilishwa na Kiongozi wa Walio Wachache katika Bunge hili la Kaunti ya Lamu.

Madam Speaker, sababu kuu ya kuunga mkono mswada huu ni kwamba masuala ya maadili (ethics) katika utumishi wa umma yamekuwa na changamoto kubwa katika kaunti yetu ya Lamu. Kumekuwa na tabia ya baadhi ya maafisa wa serikali kujiingiza katika siasa ilhali hawastahili kufanya hivyo.

Madam Speaker, maafisa hawa—wakiwemo mawaziri wa kaunti, chief officers, na ward administrators—waliidhinishwa na Bunge hili kuhudumia wananchi wote wa Lamu bila ubaguzi. Wanapojihusisha na siasa za upendeleo,

wanapoteza uzalendo na kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa haki, usawa na weledi.

Ni jambo la kusikitisha, Madam Speaker, kuona baadhi yao wakijihusisha na kampeni za kisiasa kwa niaba ya watu fulani, au hata kujitangaza wao wenyewe. Hali hii si ya kisheria wala haikubaliki. Pale ambapo afisa wa umma ameonyesha nia ya kisiasa waziwazi, inafaa kisheria ajiuzulu ili kutoa nafasi kwa utekelezaji wa haki wa majukumu ya umma.

Madam Speaker, mfanyakazi wa serikali anapaswa kuzingatia wajibu wake kama alivyoajiriwa, na si kutumia nafasi yake kushiriki katika siasa.

Kwa msingi huo, ninaunga mkono mswada huu kwa dhati. Hali inayoendelea kwa sasa hairidhishi, na Bunge hili lina wajibu wa kuchukua hatua. Tuna ushahidi, ikiwemo video, unaoonyesha mienendo hii, na tunaweza kutumia mamlaka ya Bunge hili kuwaita wahusika, hasa wale tuliowathibitisha kama chief officers na mawaziri, ili kuwajibika.

Vilevile, tunaomba kupitia uongozi wako, Madam Speaker, kwamba hoja hii itekelezwe ipasavyo na County Secretary pamoja na Public Service Board ili kurejesha nidhamu na maadili katika utumishi wa umma.

Kwa kumalizia, napendekeza kwamba maafisa wote wa serikali ya kaunti—akiwemo CCM, chief officers, ward administrators, pamoja na wafanyakazi wa kusaidia kama madereva—wakumbuke kuwa wameajiriwa kuhudumia wananchi wote bila upendeleo.

Asante, Madam Speaker.

Members Contribution

Hon. Deko Barisa Bana(Basuba): Asante sana, Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia fursa hii ili nami niweze kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kumekuwa na changamoto kubwa ambapo baadhi ya watu wanatumia ofisi za umma vibaya. Tumeshuhudia hali ambapo mtu anajitambulisha kama mtumishi wa umma, lakini wakati huo huo anajihusisha moja kwa moja na siasa.

Mheshimiwa Spika, hata mimi binafsi nimekumbana na hali kama hii katika wodi ya Basuba, ambapo mfanyakazi wa serikali, kama vile dereva, anaanza kujipambanua kisiasa na hata kujipa hadhi ambayo si yake. Hii inaleta mkanganyiko kwa wananchi na inaathiri utoaji wa huduma, kwa sababu badala ya kuwatumikia wananchi ipasavyo, anajikita katika masuala ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kila mtu ajue nafasi yake. Ikiwa mtu ameamua kuingia katika siasa, basi afanye hivyo kwa kufuata utaratibu wa kisheria—ajiuzulu kwanza kutoka katika nafasi ya utumishi wa umma.

Haiwezekani, Mheshimiwa Spika, mtu kuvaa kofia mbili kwa wakati mmoja—kuwa mtumishi wa umma na mwanasiasa kwa pamoja. Hali hii inaleta mgongano wa maslahi na kudhoofisha imani ya wananchi kwa serikali.

Kwa hivyo, Mheshimiwa Spika, mtu yeyote anayetamani kuingia katika siasa achukue hatua ya kujiuzulu na aingie kikamilifu katika ulingo wa kisiasa akiwa tayari kukabiliana na changamoto zake.

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kuongeza. Nimesimama kuunga mkono hoja hii na naomba Bunge hili liipitishe.

Asante, Mheshimiwa Spika.

Hon. Amina Hassan Bwanamkuu(Nominated): Asante, Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, nami nasimama kuunga mkono mswada huu ambao, kwa maoni yangu, umeletwa kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba mfanyakazi wa serikali hapaswi kujihusisha na masuala ya kisiasa. Ni lazima achague upande mmoja—ama abaki katika utumishi wa umma au aingie katika siasa. Haiwezekani kuendesha majukumu haya mawili kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, hali hii imekuwa ikijitokeza hapa katika kaunti yetu ya Lamu, hususan miongoni mwa maafisa wa upande wa utendaji (Executive), ambapo baadhi yao wanajihusisha na siasa kinyume na maadili ya utumishi wa umma.

Zaidi ya hayo, Mheshimiwa Spika, kumekuwa na matumizi ya rasilimali za serikali kwa shughuli za kisiasa, jambo ambalo halikubaliki hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kanuni na maadili ya utumishi wa umma hayaruhusu mfanyakazi wa serikali kushiriki katika siasa, na mwenendo huu unaathiri pakubwa utendaji kazi pamoja na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kwa hivyo, Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono mswada huu na naomba Bunge hili liupitishe ili kurejesha nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma.

Asante, Mheshimiwa Spika.

Hon. John Mburu Gitonga(Hongwe): Asante sana, Madam Speaker, kwa kunipa nafasi hii. Nimesimama kuunga mkono hoja iliyowasilishwa mbele ya Bunge hili. Ni kweli kwamba watumishi wa umma hawafai kujihusisha na siasa wakiwa bado wanahudumu serikalini.

Madam Speaker, katika kaunti yetu, tumeona hali ambapo baadhi ya watumishi wa umma wameacha majukumu yao na kujikita katika siasa. Wengine

wanashiriki kampeni, wengine wanashawishi kisiasa, na wengine wanajiandaa kugombea ilhali bado wanatumia ofisi za umma.

Hii imepelekea kudorora kwa huduma kwa wananchi. Badala ya kuhudumia wananchi, wanatumia muda na rasilimali za serikali kujijenga kisiasa. Hili halikubaliki.

Ni vyema mtu achague moja—ama utumishi wa umma au siasa. Haiwezekani kuchanganya yote mawili kwa manufaa binafsi.

Zaidi ya hayo, ni makosa makubwa kutumia rasilimali za serikali ya kaunti kwa maslahi ya kisiasa. Mali hizo ni za wananchi na zinapaswa kutumika kuwahudumia.

Naomba Bunge hili lichukue hatua madhubuti dhidi ya wale wote wanaokiuka sheria hii, ikiwemo Chief Officers na Mawaziri wanaojihusisha na siasa kinyume cha sheria.

Naomba kuwasilisha. Asante sana, Madam Speaker.

Hon.Suleiman Mohamed Farah(Witu): Asante sana, Madam Speaker.

Nami pia nimesimama kuunga mkono hoja hii muhimu. Ni jambo la kusikitisha kuona kuwa baadhi ya watumishi wa serikali ya kaunti wamejikita katika siasa na kusahau majukumu yao ya msingi.

Madam Speaker, kumekuwa na matukio ambapo hata watumishi wa ngazi za chini kama madereva wanajihusisha na siasa hadi kufikia kuwatusi Waheshimiwa MCAs mitandaoni. Hii inaonyesha wazi kukosekana kwa nidhamu katika utumishi wa umma.

Wananchi wanapoona hali hii, wanaanza kupoteza imani na viongozi wao. Sisi kama MCAs tulichaguliwa kuwatetea wananchi, lakini inasikitisha kuona wale

tuliowaidhinisha wanatupuuza na hata kupambana nasi kisiasa katika maeneo yetu.

Ni muhimu kuweka mipaka iliyo wazi: yeyote anayetaka kujihusisha na siasa ajiuzulu kwanza. Na yule anayetaka kuhudumu wananchi afanye hivyo kikamilifu bila kuingilia siasa.

Kwa kuwa muda wa uchaguzi unakaribia, ni vyema kila mmoja afanye maamuzi mapema badala ya kuharibu utumishi wa umma.

Naunga mkono hoja hii na naomba hatua zichukuliwe mara moja.

Asante sana, Madam Speaker.

Mover's Response

Hon. Fahd Dini Adnan(Minority Leader): Napenda kuwashukuru Waheshimiwa wote waliotoa michango yao kuhusu hoja hii. Ni wazi kuwa hii ni hoja ya maana sana, na ikipitishwa ni lazima ifuatiliwe kwa umakini mkubwa. Utekelezaji wake unapaswa kufuatiliwa na Ofisi ya County Secretary pamoja na County Public Service Board ili kuhakikisha maazimio ya Bunge hili yanatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kuona baadhi ya Mawaziri wikipuuza majukumu yao na badala yake kujihusisha na siasa. Idara zimezorota, hasa idara ya afya, ambapo wananchi wameendelea kulalamika kuhusu huduma duni.

Haiwezekani Waziri wa idara moja kuacha majukumu yake na kuhamahama katika idara nyingine kwa ajili ya kujijenga kisiasa. Hii ni matumizi mabaya ya rasilimali za umma na ni lazima ikomeshwe.

Pia, tumeshuhudia hali ambapo MCAs wanapotoa maoni yao, wanapingwa na watumishi wa serikali kwa misingi ya kisiasa. Hili halikubaliki.

Ni lazima tuseme wazi: yeyote anayetaka kujihusisha na siasa ajiuzulu. Na yule anayetaka kuhudumu wananchi abaki ofisini atekeleze majukumu yake kikamilifu.

Kwa hayo, nawashukuru Waheshimiwa wote kwa michango yao.

Asante sana.

(Questions put and Agreed Upon)

Speaker (Hon. Paul Njuguna Kimani): Honorable Members, there being no other business, the Assembly stands adjourned until today in Afternoon, 15th April 2026 at 2:30 pm.

The Assembly rose at 12:30p.m.